

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

08 MEI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 08 MEI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA AFYA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

277. MHESHIMIWA ADO SHAIBU ADO (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ipi kauli ya Serikali juu ya Fao la kujitoa kwa Waajiriwa na lini Serikali inafikiria kuanzisha Fao hilo.

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

278. MHESHIMIWA DOUGRAS DIDAS MASSABURI (KIVULE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara na Madaraja kutokea Pugu – Majohe, Viwege hadi Mbondole na Msongola kwa Kiwango cha lami.

279. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuigawa Kata ya Mwangeza ili kusogeza huduma za kijamii na kiutawala karibu na Wananchi.

280. MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Kata ya Manolo yenye idadi ya Wakazi 26,000 itagawanywa.

OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):

281. MHESHIMIWA LUCY EDWARD MWAKYEMBE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana):-

Je, Serikali inaboresha vipi upatikanaji wa Mitaji na Mafunzo ya Biashara kwa Vijana.

WIZARA YA UCHUKUZI:

282. MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (SONGEA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Jengo la Abiria Uwanja wa Ndege wa Songea.

WIZARA YA KILIMO:

283. MHESHIMIWA ENG. RAMADHANI HAMZA SINGANO (BUMBULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kitafiti wa kuhakikisha fursa ya kilimo cha umwagiliaji inapewa kipaumbele kwa Kata za Bumbuli.

WIZARA YA NISHATI:

284. MHESHIMIWA ASHA OMAR RASHID (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha upatikanaji wa Nishati ya gesi Vijijini.

WIZARA YA UJENZI:

285. MHESHIMIWA JOSHUA SAMWEL NASSARI (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kutengeneza Barabara ya *Bypass* Tengeru – Mererani Mkoani Arusha.

286. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Ujenzi wa Barabara ya Kyetema - Kanazi - Ibwera - Katoro hadi Kyaka ambayo ipo kwenye Ilani ya CCM kwa mara ya pili utaanza.

287. MHESHIMIWA SHAFFIN AHMEDALI SUMAR (UYUI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Tabora Mjini - Ibiri - Usagali hadi Wilaya ya Ulyankulu kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

288. MHESHIMIWA ENG. AMOSY WILLIAM MAGANGA (SIKONGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi mpya ya Polisi Wilaya ya Sikonge.

289. MHESHIMIWA OTHMAN MAULID SULEIMAN (MAHONDA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali haioni haja ya kuweka Namba ya NIDA kwenye Cheti cha kuzaliwa kuliko kusubiri mtu mpaka atimize miaka 18.

WIZARA YA MAJI:

290. MHESHIMIWA CHARLES JACOB SUNGURA (HANDENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji wa Segera – Kabuku wenye thamani ya Shilingi Bilioni 25.

291. MHESHIMIWA MARY DANIEL SURATI (SERENGETI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaongeza Bajeti ya Huduma za Maji Wilaya ya Serengeti.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
08 MEI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**